JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Boma Road,
S.L.P. 484,
SINGIDA,
Barua Pepe: rbcsingida@pccb.go.tz.
TANZANIA.
www.pccb.go.tz

SINGIDA – JULAI 17, 2020

TAARIFA KWA UMMA
HAKIMU NA DAKTARI MBARONI KWA RUSHWA

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa TAKUKURU ni chombo chenye dhamana ya kusimamia Mapambano Dhidi ya Rushwa Nchini tukiongozwa na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007.

Ifuatayo ni Taarifa kwa Umma inayoonesha Utendaji kazi wa TAKUKURU Mkoa wa SINGIDA kwa kipindi cha Aprili – Juni, 2020 pamoja na mikakati tuliyojiwekea kwa kipindi cha Julai – Septemba, 2020.

1. UCHUNGUZI

Katika dawati la uchunguzi kipindi cha April – June 2020 TAKUKURU Mkoa wa Singida tuliweza kutekeleza mambo yafuatayo:-

A. KESI

Jumla ya kesi 8 zenye watuhumiwa kumi na saba (17) zimefikishwa mahakamani na kufunguliwa mashauri ya jinai.

Mchanganuo wa kesi hizo ni kama ifuatavyo:-

i. Kesi ya Jinai Namba 05 ya Mwaka 2020 Mshtakiwa ni TATU MWENDA MBUA Mwenyekiti wa baraza la ardhi kata ya Puma Wilayani Ikungi na wenzake sita (6) ambao ni wajumbe wa baraza hilo wanatuhumiwa kuomba Rushwa ya Tsh. 100,000/= na kupokea Tsh. 50,000/= ili watoe ushindi kwenye kesi ya shamba kwa mtoa taarifa ambaye jina lake limehifadhiwa.

ii. Kesi ya Jinai Namba 07 ya Mwaka 2020 mtuhumiwa ni Dr. ABDUL HUSSEIN SEWANDO wa Hospital ya Mkoa wa Singida, ambaye aliomba na kupokea hongo ya Tsh. 60,000/= kutoka kwa mgonjwa (Jina limehifadhiwa) ili amfanyie huduma ya vipimo vya 'Ultra Sound".

iii. Kesi ya Jinai Namba 06 ya Mwaka 2020 Watuhumiwa ni RAJABU SHABANI KASSIM, huyu ni Mlinzi wa Kampuni ya "Intelligence" na JOSEPH SELESTINE MAGULYATI (Mjasiriamali) hawa kwa pamoja wanatuhumiwa kutoa hongo ya Tsh 500,000/= kwa Mtendaji na Mwenyekiti wa kijiji cha Nkinto huko Wilayani Mkalama ili kiwe kishawishi cha kuwaandikia muhtasari wa kughushi kuwaonyesha kuwa waliuziwa na kijiji hicho eneo ambalo lina mnara wa kampuni ya Vodacom.

iv. Kesi ya Jinai namba 27 ya Mwaka 2020 mtuhumiwa ni SAMMY EDWARD LAZARO na MUSSA PATRICK MALALA hawa ni wakusanya ushuru wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ambao waliomba na kupokea Tsh. 50,000/= ili asimtoze faini mlalamikaji aliyetuhumiwa kwa kusafirisha kuku kwenye gari la abiria (basi).

v. Kesi ya Jinai Namba 82 ya Mwaka 2020 watuhumiwa ni ALBERT MUSTAPHA NGIMBA ambaye ni Afisa Elimu Vifaa na Takwimu wa Wilaya ya Iramba na GEORGE MKOKOMA MNEBWA ambaye ni

Mwl. Mkuu wa shule ya msingi Isenenkwa hawa wanatuhumiwa kumhonga Tsh 500,000/= afisa wa TAKUKURU ili aharibu uchunguzi wa miradi ya umaliziaji wa vyumba vya walimu na matundu ya vyoo uliokuwa unaendelea.

vi. Kesi ya Jinai Namba 74 ya Mwaka 2020 kesi hii inawahusu Mh. BAHATI MANONGI ILIKUNDA wa mahakama ya mwanzo Kilimatinde Wilayani Manyoni ambaye aliomba Tsh. 350,000/= na kupokea Tsh. 170,000/= kupitia kwa mwenza wake Bw. HAJI JUMA BWEGEGE ambaye kwenye shauri hili naye ni mtuhumiwa. Mh. Manongi aliomba fedha hizo ili atoe upendeleo kwa mwananchi mmoja ambaye alikuwa na shauri la madai lililokuwa mbele yake.

vii. Kesi ya Jinai Namba 79 ya Mwaka 2020 mtuhumiwa JOHN NASON YAKO ambaye ni Afisa mifugo msaidizi daraja la II huko Wilayani Mkalama, huyu aliomba na kupokea Rushwa ya Tsh 20,000/= toka kwa mwananchi mmoja ili asimchukulie hatua kwa kumtuhumu kuwa alichinja na kuuza nyama ya ng`ombe pasipo kupimwa.

viii. Kesi ya Jinai Namba 58 ya Mwaka 2020 watuhumiwa ni NASSORO SONGERAEL NALUGWA (Mwenyekiti wa Baraza la kata la Old Kiomboi), JAREDI ANTHONY KITUNDU (Katibu wa baraza) na DANIEL KINGU MSENGI (mjumbe) ambao waliomba rushwa ya Tshs. 400,000/= na kupokea rushwa ya Tshs. 22,000/= kwa njia ya tigopesa ili waweze kumsaidia mtoa taarifa kwenye kesi yake ya madai ambayo iko mbele ya baraza hilo.

B. FEDHA ZILIZOOKELEWA

Kiasi cha shilingi 136,111,210/= zimeokolewa kwa kipindi cha Mwezi Aprili hadi Juni kwa mchanganuo ufuatao:-

i. Sh. 34,196,610 kiasi hiki kimeokolewa kutokana na vifaa vya mfuko wa jimbo vilivyokuwa vimenunuliwa pasipo kukabidhiwa bohari ya Halmashauri, kuwasilishwa halmashauri.

ii. Sh. 16,000,000/= fedha hizi zimerejeshwa kwa wananchi 8 wa Wilaya ya Ikungi ambao walibambikwa kesi kisha kulipishwa faini.

iii. Sh. 13,581,600/= hizi zilikuwa fedha za AMCOS ya Jikomboe Wilayani Iramba ambazo zilikuwa hazijalipwa kwa wakulima wa pamba baada ya kuchepushwa na wajumbe wa bodi.

iv. Sh. 7,086,000/= fedha hizi ziliokolewa baada ya wakusanya ushuru kutoziwasilisha Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi hadi pale TAKUKURU ilipofanya uchunguzi na kuzirejesha fedha hizo Halmashauri husika.

v. Sh. 4,000,000/= fedha hizo zilirejeshwa na TAKUKURU kwa jumuiya ya watumia maji kijiji cha Mkulu Wilayani Iramba baada ya viongozi wa jumuiya hiyo kuzichepusha.

vi. Sh. 1,700,000/= fedha hizi ni za ushuru zilikuwa za MSAI AMCOS iliyopo Wilayani Iramba zilichepushwa na wajumbe wa bodi.

vii. Sh. 20,547,000/= ziliokolewa kutoka kwenye vyama vya Ushirika, Wilaya za Singida, Ikungi na Mkalama.

viii. LOTH JOHN MWANGU Mstaafu huyu ambaye alikuwa mwalimu wa Shule ya Msingi Ilongo Halmashauri ya Mkalama tarehe 15/07/2016 alikopa Tsh. 9,000,000/= toka kwa mkopeshaji ajulikanaye kwa jina la Bhoke ambapo tarehe 03/02/2017 baada ya kupata mafao yake

alirejesha Tsh. 22,500,000/= tarehe 20/06/2020 Ofisi ilifanikiwa kumrejeshea Tsh. 13,500,000/=.

ix. SELEMAN HAJI TYEA Mstaafu huyu ambaye alikuwa Mwalimu wa Shule ya Msingi Endasiku Halmashauri ya Wilaya Mkalama tarehe 16/05/2016 alikopa Tsh. 2,000,000/= kwa mkopeshaji ajulikanaye kwa jina la Bhoke, Disemba, 2016 alirejesha Tsh. 24,000,000/= Tarehe 20/06/2020 Ofisi ya TAKUKURU imefanikiwa kumrejeshea Mhanga Tsh. 22,000,000/=

x. MAGRETH BUSONGO Mstaafu huyu ambaye alikuwa Muuguzi alikopa Tsh. 1,000,000/= toka kwa Angeliver Financial LTD ya Wilayani Iramba kisha ndani ya miezi minne alirejesha Tsh. 9,250,000/= hadi sasa juhudi za TAKUKURU zimefanikiwa kumrejeshea Mhanga Tsh. 3,500,000/=.

2. ELIMU KWA UMMA

Katika utekelezaji wa majukumu yake TAKUKURU (M) wa Singida iliendelea na jitihada za kuelimisha umma kuhusu haki na wajibu wa wananchi katika mapambano dhidi ya Rushwa kwatika kipindi cha mwezi Aprili hadi June, 2020 mada kuu ikiwa ni Athari za Rushwa kwenye jamii na madhara ya Rushwa ya Ngono vyuoni.

Katika kipindi tajwa jumla ya semina 04 zimefanyika, Vipindi vya redio 04, habari zilizotolewa na vyombo vya habari 03 na wanafunzi wa vyuo walielimishwa kuhusu madhara ya Rushwa ya ngono vyuoni. Vyuo vinne vilifikiwa ambavyo ni Chuo cha Uhasibu TIA, Chuo cha Utumishi wa Umma, Chuo cha Maabara na Chuo cha Ualimu Singida na jumla ya wanachuo 634 walipewa mafunzo hayo.

3. UZUIAJI RUSHWA

Katika kuthibiti mianya ya Rushwa kipindi cha Aprili hadi June, 2020 TAKUKURU (M) Singida ilifanya ufuatiliaji wa Miradi ya maji na ujenzi wa Karakana ya Mifugo Chuo cha Ufundi VETA Singida. Pia ulifanyika uchambuzi wa mifumo kuhusu udhibiti wa mianya ya Rushwa katika utatuzi wa migogoro ya ardhi katika Mabaraza ya Kata na Vijiji kwa Wilaya ya Singida na Uchambuzi wa mfumo kuhusu mianya ya Rushwa katika utoaji wa Bima ya Maisha wa Shirika la Bima la Singida.

4. MKAKATI WA UTENDAJI KAZI KUANZIA JULAI – SEPTEMBA, 2020

Mkakati wa utendaji kazi TAKUKURU (M) wa Singida katika robo ya kwanza ya mwaka inayoanzia Julai hadi Septemba, **2020** ni kuendela kufanya uchunguzi kwa taarifa zote za vitendo vya Rushwa zitakazoibuliwa, kufanya uelimishaji kwa jamii kuhusiana na madhara ya rushwa hasa katika Uchaguzi Mkuu wa **2020**, ufuatiliaji wa kina katika miradi ya maji na elimu kwa lengo la kuona uwiano wa fedha zilizotolewa na Serikali na majengo yanayojengwa au manunuzi ya vifaa.

Tunawasihi Wananchi waendelee kushirikiana nasi kwenye mapambano dhidi ya Rushwa kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka **2020**.

Imetolewa na :

ADILI ELINIPENDA
MKUU WA TAKUKURU (M)
SINGIDA